

Jiwe la kiroho la kujengea na 164

JITAMBUE WEWE U NANI!

Wagalatia 4:4-7, “Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa mwanawe mioyoni mwetu aliaye, Aba, yaani baba. Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu kwa njia ya Kristo.

Sikilizeni kile Nabii wa Mungu ndugu, Branham alichosema juu ya hilo:

Mara nyingi nimesema, nakutana na watu wa aina mbili katika wakati ninapozunguka dunia kwa huduma ya umisheni. Nakutana na watu aina mbili moja ni wapentecoste na wapili (wakristo) wa kimsingi.

Hawa wa kimsingi wanajua wanaposimamia. Nao wanalichukuwa kwa Neno. “Mimi ni mwana wa Mungu kwa (kukiri) kuungama kwangu” Unaona? Yeye anachukuwa msimamo huo, wanajua mahali pao, lakini hana imani au imani itoshayo, juu ya kile anachozungumzia. Wapentecoste wanayo Imani ya kutosha, lakini hawajui wanaposimamia. Hajui yeye ni nani au wao ni nani.

Ni kama tu mtu aliye na pesa katika benki, naye hajui namna ya kuandika cheki. Na yule mwingine anaweza kuandika cheki lakini hana pesa katika benki [1].

Kama unaweza kuwaleta wao pamoja, utazipata kama tu watajitambua wao ni nani. Ninyi ni wana na mabinti za Mungu, siyo mtakuwa, warithi wa ufalme. Sasa hivi tu wafalme (Ufunuo 1:56-6). Dai haki zako za kisheria. Usiache shetani akukandamize na chochote juu yako. Wewe ni wa Mungu na hanayo haki ya kushikilia chochote.

Kila mmoja anaangalia siku zote Dalili zao. Mchungaji atawaombea wao. Wanaenda na kusema, “Vema, unaona bado sijisikii vizuri” Vema, huo sio uponyaji. Dalili ni jambo baya mno ambalo.....Hilo ni moja ya mambo ya kuogopesha ambayo shetani anayatumia. Dalili hazina uhusiano na hilo. Ni kwa sababu Mungu amesema hivyo.

Oh, jamani kama kuna mtu aliyekuwa na Dalili, ilikuwa ni Yona yeye alipaswa kuwa na Dalili, alikuwa amerudi nyuma, mikono imefungwa nyuma yake, katika tumbo la samaki, akiwa ndani ya maji kiasi cha maili moja baharini, katika bahari yenye dhoruba, majani ya bahari yakizunguka shingoni mwake. Zungumzia Dalili, akiangalia upande huu ni tumbo la samaki, akigeuka upande huu ni tumbo la samaki, Kila upande aliogeukia ilikuwa tumbo la samaki. Lakini alisema, hayo yote ni ubatili udanganyao (Yonah 2/1, Wafalme 9:1-3)

hiyo ni kweli. Alisema, “sitaangalia hili tumbo la samaki tena, lakini mara nyingine tena nitaangalia hekalu lako takatifu, Bwana” inategemea unaangalia nini. Kama unaangalia Dalili zako, zitakuwa pale. Kama unaangalia neno la Mungu, Dalili zote itabidi ziondoke.

Kwa nini Yona alifanya hivyo? Kwa sababu alijua Sulemani alipoliweka wakfu lile hekalu takatifu, alisema, “Bwana, kama watoto wako wakiwa shidani mahali popote nao wataangalia kuelekea hekalu hili na kuomba, hapo sasa usikie kutoka mbinguni (2 Nyakati 7:11-17). [2]

Sikiliza, ninyi ni watu mlio na Agano na Mungu. Mungu alimkatakata vipande Kristo pale msalabani, akilifanya Agano, akiapa kwa yeye mwenyewe. Na akauchukua ule mwili juu mbinguni, ambao siku moja utarudi. Lakini Roho alimtuma tena kuliongoza kanisa (Matendo 2:1-4) uhai ule ule uliokuwa ndani ya Kristo Yesu

uko ndani ya kanisa usiku wa leo kwa njia ya Roho Mtakatifu, akitenda, na kufanya na kutimiza mambo yale yale Aliyoyafanya alipokuwa hapa duniani umeupokea huo. Unalo Agano. Limeandikiwa wewe, na Mungu akaapa. Huwezi ukashindwa. Hilo linamfanya shetani achanganyikiwe; hakika linamfanya hivyo, unapojua/unapojitambua wewe ni nani.

Ninachotaribu kufanya ni kuwafanya watu wajitambue wao ni nani. Unaona? Kama tu ungejua wewe ni nani usiku wa leo. Kutakuja mtiririko wa imani hapa, mpaka pasiwepo mgonjwa hata mmoja. Hakutakuwepo na haja ya mstari wa maombi, kama watu waliopo hapa watatambua wao ni nani. Hivyo ndiyo njia pakee uwezayo kufanya.

Unafikiri ikoje katika nchi za kigeni, kutembea na kupigana na nguvu za mapepo (giza) na kila kitu?.

Inabidi ujue unaposimamia shetani hajali unapiga kelele kwa nguvu kiasi gani. Shetani hajali unarukaruka vipi juu na chini. Shetani atashikilia hapo. Lakini inabidi aitambue Imani. Itamtoa yeye wakati wowote. Kwa hiyo hapo ndipo ilipo leo.

Kanisa linazo baraka (Effeso 1:3) lakini halijui hivyo [3] Yesu Kristo mwana wa Mungu, yeye alikuwa Neno la Mungu hapa duniani. Tunajua kwamba alikuwa Neno la Mungu. “hapo mwar² lilikuwepo Neno, Naye Neno akafanyika mwili alikaa miongoni mwetu” (Yohana 1:1-3,14). Watu leo wanajaribu kumlinganisha Yesu Kristo na nabii. Yeye alikuwa zaidi ya nabii. Alikuwa ni Emmanueli (Matayo 1:21-23). Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake (2 Kor 5:17-19). Alikuwa ni Mungu mwenyewe akidhihirishwa katika mwili au sivyo mdanganyifu mkuu aliyewahi kuwapo duniani. Alikuwa ni Mungu alikuwa vyote viwili mtu na Mungu.

Alipokuwa anatokea mlimani, kama mwanadamu aliona njaa, alipouona mti aliuangalia aone tini na hakukuwa na tini, na Alisema, “mtu asile matunda kwako”, aligeuka na akaenda zake (Marko 11:12-14 na 20 – 21).

Nashangaa kwa nini hakukaa nakusubiri aone kama ule mti utaenda kukauka au hapana! Yesu aliufanyia nini huo mti? Yeye aliuita ule uhai wake utoke ndani yake hukungoja ili aone utakauka au hapana alijua utakauka; Alishasema hivyo. Na neno la Mungu lilikuwa ndani yake na chochote Alichosema, Lazima kitimie/kitokee kwa sababu ilikuwa ni Mungu akizungumza kutoka kwa mwanadamu. Na kila kitu alichu Mungu, Mungu alikimwaga kwa utimilifu wote ndani ya Yesu Kristo. Na kila kitu Yesu Kristo alichokuwa, Alikimwaga ndani ya kanisa.

Na hiyo ndiyo shida iliyo kwenye kanisa la Pentecoste usiku wa leo, wale wanaoamini Neno lote, hawajajitambua wao ni nani. Hawaelewi ile nguvuiliyo ndani ya jengo hili usiku wa leo, Lakini inapotelea chini kwa kutokuamini (1 Kor 4:20). Hilo ndilo jambo pekee. Kama Mungu angepata mahali pa kufanyia kazi kupitia wewe, ingekuwa ni makuu sana ambayo angefanya lakini inapotea hatuipi nafasi, tunaizuia kwa sababu ya kutokuamini. [4].

Wapentecoste wamepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na hiyo inawafanya wao kuwa sehemu ya ushirika katika uhusiano wao na Mungu, wale waliozaliwa mara ya pili, ni wana na binti za Mungu. Waambie wao kitu kutoka katika Biblia nao wataamini.

Lakini jambo lililopo, wanasahau wao ni nani. Wanafikiri, “Vema sijui” oh, ndugu, ninyi ambao mmezaliwa mara ya pili ni wana na binti za Mungu (1 Yoh 4:4), ni washirika sawa na Yesu Kristo, katika

uwepo wake. Oh, jamani hilo ndilo linalomfanya shetani akasirike kule kulifanya kanisa la Mungu litambue wao ni nani.

Oh, ninyi kanisa kuu la Mungu aliyehai, unapaswa.....Ninyi mnaodai mmezibusu baraka kutoka katika kikombe, wakati mwingine nashangaa kama Mungu atachukua injili yake na kuwatingisha mfike mahali mapaka mjitambue ninyi ni nani, na zile haki mlizonazo, mambo mliyojaliwa na Mungu.

Shetani hana haki ya kitu chochote yeye ni mtishiaji. Alir³ ;'anywa kila kitu alichokuwa nacho pale Msalabani, wakati Yesu Kristo alipochukuwa nafasi ya mwenye dhambi na akafa pale msalabani (Wakolosai 2:13-15) Shetani hana haki ya kisheria juu ya chochote tena. Halleluya. Lakini kilakitu kiko mkononi mwa kanisa na mwaminio. Liko hivyo, shetani

amepoteza yeye sio chochote bali ni mtishiaji.

Hata mauti yenyewe, ambayo tumehubiri usiku uliopita.....Yule nyuki anapoteza ule msumari wa kuchomea, bado ni nyuki, lakini hana msumari wa kuchomea. Na kifo hakina uchungu kwa mwaminio, uchungu umeondoka (1 kor 15:51-57). Kifo kinazunguka karibu, kikisema. “Vema huu ni mwisho wa safari” Naweza kuelekea msalabani na kuonyesha ufufuo Halleluya. [5]

Na tunajihesabu wenyewe kwamba tumekufa (Warumi 6:11). Tumezikwa pamoja naye katika ubatizo katika mauti yake na tumeinuka naye katika kufufuka kwake (Warumi 6:3-4). Na sasa hivi tumeshaingia tayari, sio tutaingia tumeshainuka tayari, oh, jamani tumeshaingia sasa, sio tuta; tumefika sasa, usiku, tukiwa tumeketi katika ulimwengu wa Roho kwa vipi? Ndani ya Kristo Yesu

(Efeso 2:4) siyo tutakuwa wakati mwingine tuko hivyo sasa Kanisa halijitambui kuwa ni nani, unaona? Tuko hivyo sasa, dakika hii sasa kwa jinsi gani? Ndani ya Kristo Yesu, tukiwa tumekusanyika pamoja ndani yake, tukiwa tumeinuliwa kutoka kwa wafu. Nafsi zetu ni zisizokufa. [6]

Katika ulimwengu wa kiroho oh jinsi nitamanivyo kama ninge kuwa na muda. Liko hapa nimeliwekea alama hasa, hapa katika Biblia yangu kuhusu ulimwengu wa kiroho. Ni nini ulimwengu wa kiroho? Ulimwengu wa kiroho (mahali paki Mbinguni) ni nafasi ya mwaminio ndani ya Kristo, pale mwaminio anaposimama ndani ya Kristo, katika mahali paki Mbinguni (ulimwengu wa Roho). [7].

Na nguvu ileile, Kristo yuleyule.....Haleluya wacha wanaotegemea kanuni waache wasioamini nguvu za Mungu waseme sio sahihi; lakini nguvu ile ile iliyonena dunia ikawepo iko

ndani ya watu ambao wana Roho Mtakatifu (Mwanzo 1:3). Hiyo ni kweli wanaume na wanawake, huu ni wakati wa kujitambua wewe ni nani?

Shetani anajaribu kukufichia nyuma, akikuambia wewe ni mtu mdogo tu wa kukanyagwakanyagwa. Sivyo ulivyo. Ninyi ni wana na binti za Mungu uungu hauko Mbinguni; uko ndani yenu haleluyah.

Ninajua mnafikiri nimerukwa na akili, lakini ngoja niwaambie jambo fulani, ndugu unapotambua yakuwa Mungu mwenye nguvu zote anaishi nda ⁴ uko, hilo ni vema tu, “uzima wangu, ninawapa uzima wa milele (zoe) uhai uzima wa Mungu uhai wa Mungu uko ndani ya wanadamu (Yoha 14:15-20)

Sasa marafiki. Ninajua hii ni kweli ninajua watu hawajitambui wao ni nani! Kila mmoja hapa anaweza akaishi juu ya dhambi, anaweza kuishi bila dhambi (1 Yoh

5:18-19) ishi ndani ya Mungu; utafanya makosa, lakini damu ya Kristo itakusamehe wewe (1 Yoh 1:9) “Baba wasamehe wao, kwa maana hawajui watendalo” Hiyo ni kweli?

Nguvu ile ile ya Kristo iliyotundikwa pale msalabani, Mungu yuleyule aliyemfufua yeye katika siku ile ya ufufuo, yuko ndani yako sasa, Ninyi mlio na Roho Mtakatifu oh, hamumpendi yeye? Oh, jamani sikieni sauti yake ikiita leo. [8]

Yesu, Alikuwa ni Neno na alikuwa na imani na nguvu zake. Ni kwa namna gani? Alisema, siwezi kufanya lolote kwa nafsi yangu (Yoh 5:19) kwa nini? Alitegemea kile alichokuwa; alijitegemea ufahamu wake wa kutambua kuwa Yeye alikuwa Neno. Na alikuwa na imani katika Mungu, aliyemfanya yeye kuwa Neno. Alikuwa Mungu Neno, na lilikuwa ndani yake na hilo lilimpa yeye imani, kwa sababu alitambua nafasi yake. Alijua kile

alichokuwa, kwa sababu maandiko yalisema Yeye alikuwa hivyo (Luka 24:25-27).

Na hapa kila andiko lilikubaliana na lingine kuthibitisha kwamba Yeye alikuwa hasa kile maandiko yalisema Yeye atakuwa, na alijua Yeye alikuwa nani.

Kwa hiyo alitegemea kile Mungu alichomfanya Yeye kuwa na kama Yeye alifanya hivyo, hatuwezi nasi kutegemea kile Mungu alichotufanya kama waaminio? “ Ishara hizi zitaambatana nao waaminio” (Marko 16:17-18). Alikuwa na imani na kile alichokuwa, na kama ni mwaminio, kuwa na imani kwa kile ulicho wewe ni mwaminio na kama una imani kwa Mungu, Biblia inasema hapa.....”Kama mioyo yetu inatuhukumu hapo sasa hatuwezi kuwa na imani. Lakini kama mioyo yetu haituhukumu, hapo sasa tunayo imani; tuna imani kumuelekea Mungu”

Kama unataka kusoma hilo, linapatikana (1 Yoh 3:20-22)

Angalia kama mioyo yetu haituhukumu, basi tunao ujasiri mbele za Mungu lakini ili mradi unafanya vitu ambavyo sio sahihi, huwezi kuwa na ujasiri mbele za Mungu kwa hiyo unaona, hila shaka utatambua tu kuwa uko makosa⁵ tajiweka mwenyewe pale kama mwenye dhambi kwa kujua kwamba uko makosani lakini kama moyo wako haukuhukumu wewe, na unajua umwaminio, na hakuna chochote kati yako na Mungu, unaweza kuomba lolote utakalo na unajua kwamba utalipewa, kwa sababu ni Neno umepewa wewe kama vile ilivyokuwa kwa wanafunzi.

Sasa, njia pekee upaswayo kufanya sasa, ni kuwa na Imani kwa kile ulicho. Kuwa na Imani kwa kile Neno linachokuambia u nani. Na Yesu alikuwa na Imani kwa Neno la Mungu ambalo lilisema Yeye alikuwa ni nani, “Nimeandikiwa haya” (Luka 24:44-

47). Je Daudi katika zaburi, na manabii na wote hawakumzungumzia Yeye? “ mimi ni mkate wa uzima ambao umetoka kwa Mungu huko Mbinguni” (Yoh 6:33-35 na 48-51) Amini “ Mimi ni ule mti wa uzima kutoka bustani ya Edeni “(Mwanzo 2:9)

Mimi ni mambo haya yote; Mimi niko ambaye niko (Kutoka 3:13-15) na alijua pamoja na hilo, Imani kamilifu, kwamba alikuwa masihi aliyepakwa mafuta (Yoh 4:25-26). Kwamba Roho wa Mungu alikuwa juu yake. Alisema, “Sasa, mimi mwenyewe, siwezi kufanya lolote; lakini ni Imani yangu kwa Mungu”. Na Mungu alikuwa ndani yake, lile Neno likidhihirika na Neno la Mungu linapokuja kwako, linadhihirishwa, kwa maana wewe ni mwaminio unaona? Na mwaminio ni Imani ya Mungu ikitembea ndani yako (2 Kor 4:13; Gal 2:19-20; Mark 11:22) unapenda hilo? Napenda kufundisha hasa Imani ni nini,

Akijua Yeye ni nani, bila shaka yoyote, alijua alikuwa ni mwana wa Mungu. Alilijua hilo, kwa maana Neno lilijitambulisha. Neno la Mungu lilimtambulisha Yeye alikuwa nani. Alisema, “kama sifanyi kazi za Baba yangu, basi msiniamini; lakini kama sifanyi hizo kazi msiniamini (Yoh 10:37-38) lakini kama ninazifanya, basi aminini hizo kazi, kwa maana ni udhihirisho wa Neno lililoahidiwa” oh kama mnaweza tu kupata mwamko wa hilo kwa dakika tu. Unaona, lenyewe limemtambulisha Yeye alikuwa nani. Na alisema, Nani awezaye kunishtakia dhambi? Kwa maneno mengine. “Nani awezaye kunionyesha maisha yangu na kazi zangu kuwa hazitimizi hasa vile mesiya angelifanya? Hakuna awezaye kusema chochote; kwa maana alikuwa ndiye. Kwa sababu hiyo alikuwa na Imani kuamini kwamba chochote ambacho angelinena kingalitokea. [9]

Kama umeolewa na Kristo, Kristo ni Neno la Mungu Katika Mt. Yohana sura ya kwanza ilisema “Hapo mwanzo kulikuwepo Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu. Na Neno alikuwa Mungu na Neno alifanyika mwili na akakaa kwetu” Kristo alikuwa Neno lililohai. Siku zote Yeye alikuwa Neno na bado yeye ni Neno atabakia siku zote kuwa Yeye ni Neno. Alikuwa tu udhihirisho wa sifa za Mungu kwa maana alikuwa ni Mwana wa Mungu. [10]

Alikuwa tu ni mtu mmoja, mtu mkamilifu. Aliyatoa maisha yake, na alitoa mfano kwa ajili yako.

6

Sasa, tufanye nini? Sasa, jambo la kwanza ninalotaka kusema ni Yesu hakuishi kwa ajili yake maisha yake aliyatumia kwa ajili ya wengine huo uzima ni uzima wa milele mkamilifu unaposema unaenda kanisani na unafanya mambo mazuri, hilo ni zuri. Lakini unapoishi maisha yako kwa ajili

yako mwenyewe, huna uzima wa milele. Uzima wa milele ni kuishi kwa ajili ya wengine.

Ilithibitisha hilo alipokuja ndani ya mwanakondoo wa Mungu. Aliishi na alikuwa na uzima wa milele, kwa sababu hakuishi kwa ajili yake mwenyewe. Aliishi kwa ajili ya wengine. Na unapokea uzima wa milele kwa kuipokea siku ile, na huishi kwa ajili yako tena. Unaishi kwa ajili ya wengine mtu mmoja alisema” yawezekanaje usimame na kumwacha mtu yeyote akuite jina baya?” Huishi kwa ajili yako, unaishi kwa ajili ya wengine ili kwamba uweze kumuokoa mtu yule. Mnakuwa wana. Na shida iliyopo ni kuwa kanisa limesahau kuwa wana. Ninyi ni wana mnachukuwa mahali pa Kristo. Ninyi ni wana; kwa hiyo msiishi kwa ajili yenu wenyewe; ishi kwa ajili ya wengine.

“Vema, ndugu Branham, naweza kuishi kwa ajili ya huyu ndugu kwa kuwa ni mtu

mzuri”. Hiyo siyo. Ishi kwa ajili ya yule mtu anayekuchukia (Matayo 5:43-48). Ishi kwa ajili ya yule mtu ambaye angekuua kama angeweza. Hivyo ndivyo walivyomfanyia. Walimuua, na alikufa ili awakomboe wao. Huo ndio uzima wa milele. Hilo linapokuwa ndani yako, unaelekea Mbinguni sasa. Lakini unajitolea vitu vyako mwenyewe, unavitoea kama vile kondoo atoavyo sufu yake. Unaangalia kuelekea msalabani. [11]

Uko pale. Yesu Kristo alikufa, alikufa msalabani, na akakamilisha ukombozi (kurudisha kwa mmiliki wake wa kwanza kwa njia ya kununua au kulipa gharama) na kwa hiyo kutuweka sisi kama wana. Hakutufanya sisi kama wana, kwa maana tayari tulikuwa wana wake, lakini alituweka sisi kama wana; kwa maana ili mradi tuko duniani, katika mwili, hatuwezi kutambuliwa kama wana wake. Tulishikiliwa utumwani na shetani. Hata hivyo, tulikuwa wana. Na sikieni hili: kwa

sababu ni wana, Mungu ametuma Roho wa Mwanae katika mioyo yenu ambapo mnalia Baba, Baba, (Wagal. 4:6 – 7). Ni juu ya nani Roho Mtakatifu alishuka siku ya Pentecoste? Wana. Kule Korintho? Juu ya wana waliposikia Neno (Matendo 10:44 – 46). [12]

Lakini unapozaliwa na Roho wa Mungu, hapo sasa ni mwana wa Mungu, na siku zote ulikuwa mwana wa Mungu na siku zote utakuwa mwana wa Mungu. Hakuna njia ya kutenganisha, kwa sababu unao uzima wa milele. Na kitu cha milele hakina mwanzo wala hakina mwisho.

7
Oh, ni Neema ya Mungu kwamba Ametupa sisi kuelewa siri, hizi kuu. Kama Paulo alivyozidi kuzungumzia zaidi kule chini kwa Waefeso, akizungumzia juu ya Mume na mke alisema, “Hii ni siri kuu” Jinsi wana

wake wapaswavyo kuwaheshimu waume zao (Efeso 5:22 – 23). Hata mahali pa pili, naamini ipo katika Biblia yote ambapo kicho kilizungumziwa, alisema wanawake wawaheshimu waume zao, kicho kwa waume zao. Na mwanaume anapaswa kuishi maisha mbele ya mkewe ambayo yatamfanya huyu mwanamke amheshimu yeye kama mwana wa Mungu. Na kama haishi maisha ya aina hiyo, Vema, kwa sababu mwanamke hatamheshimu yeye, kwa sababu anajua ameumbwa na nini. Lakini kama ni mwanaume anayejiheshimu, heshima na msafi pamoja na mkewe, na mbele ya familia yake, mtumishi halisi wa Mungu, hapo sasa mwanamke, watoto, wote wanapaswa kumheshimu huyo mtumishi wa Mungu kwa kicho. [13]

Swali: Je kila mwana wa Mungu anaweza akawa na upako utoshao kiasi cha kufanya miujiza, Ishara, maajabu au ni kwa jinsi Roho Mtakatifu atakavyo elekeza?

Ndivyo ni kama tu Roho Mtakatifu atakavyo elekeza. Kama u mwana wa Mungu, au binti wa Mungu, chochote ulicho, wakati umepokea Roho Mtakatifu, hapo sasa Roho Mtakatifu anakuelekeza kufanya mambo. [14]

Sasa hivi tuko mahali pa kimbinguni. Tuko sasa hivi katika nguvu za kufufuka.

Kama hakungekuwa na sheria kwa hilo, wana na binti za Mungu wangeweza kuumba dunia yao na kuondoka hapo wakaishi maisha yao binafsi huko. Unayo nguvu ndani yako ya kufanya hilo (2 Petro 1:3 – 11) kama una kivuli kidogo tu cha nguvu za Mungu ndani yako, unayo nguvu ya kulifanya hilo. Mungu hashindwi na jambo. Unaona ninachomaanisha? Nguvu iliyo ndani yako itafanya Unaweza ukazungumza dunia ikaumbika na kwenda kuishi huko. Haleluya. Tuko hapo.

Hiyo ndiyo nguvu iliyo ndani ya Kanisa sasa (Waefeso 3:20 – 21) lakini inatawaliwa na sheria. Na hiyo sheria siyo ya kushika amri kadhaa. Ni sheria ya Imani. Yesu alisema, “Yote yanawezekana kwake aaminiye”. Na kama unaweza kuliadini hilo, chochote Mungu atakachoongoza nafsi yako kuadini hicho kitakuwa chako. Kila mahali unayo wako wa mguu utakapokanyaga kwa imani, Mungu anakupa wewe (Joshua 1:3 – 9). Amen. Hilo litakuwa lako, utalimiliki hilo. Kama unaweza kupata ufunguo kwa sheria ya Imani ambayo inakufungulia wewe. Unaona ninachomaanisha? Ile nguvu inatawaliwa na kama u mwana wa Mungu, u binti wa Mungu, hilo halikuachi kamwe.

Liko nawe wakati wote. Lakini imani yako inaenda mbali na hilo, lakini bado liko hapo . Haleluya.

Unapokuwa umeokoka, Mungu anakupa Imani ya kuinuka kutoka kwenye matope ya dunia. Imani yako inashinda mambo ya dunia. Imani yako ni nini? Imani yako ni lile tendo ambalo Mungu amekutendea ndani yako kukufanya mwana wa Mungu. Unaacha uongo wako, unaacha wizi wako, unaacha ulevi wako, kwa sababu Imani yako inainuka juu ya hilo. Amen. Kama hufanyi hilo, basi huna Imani yeyote. “Na ni kwa Imani mmeokolewa, na hiyo ni kwa Neema (Waefeso 2:8 – 9) [15]

Haijalishi umdogo kiasi gani, umkubwa kiasi gani, uwamuhimu namna gani, au sio wa muhimu, uko hapa kwa ajili ya kutumikia kusudi Fulani. Macho yangu na kila kiungo cha miili yetu kipo kwa kusudi fulani.

Na hakikuwekwa hapa kuona kitaonekanaje kitakapowekwa, lakini kimewekwa kutumikia kusudi fulani. Ilikuwa ni

mpango wa kiungu wa Mungu hufanya hivyo. Na kama tumewekwa hapo kwa makusudi (Warumi 8:28-29), kwa hiyo hakuna chochote kiwezacho kutuharibu sisi mpaka mpango wa Mungu umetimizwa. Hakuna kiwezacho kutudhuru sisi mpaka lile kusudi la Mungu lililotuweka hapa liwe limedhihirishwa.

Haijalishi tunashida kiasi gani, tunaumwa na moyo kiasi gani au tunapitia huzuni kiasi gani, yote hayo ni sababu, na kuna sababu ya hayo.

Tuchukue, kwa mfano, Nuhu katika Biblia, kulikuwa na mafuriko yaliyokuja na dunia yote iliharibiwa. Uoto wote na kila kitu kiliharibiwa ila Nuhu na ile mbegu aliyoichukuwa ndani ya safina.

Kusudi la Mungu kamwe haliwezi kushindwa. Hakuna kiwezacho kulishinda kwa hiyo tunapaswa kuwa wenye furaha leo, tukipumzika juu ya ufunuo mzuri wa

Neno la Mungu aliye hai, kwamba hakuna mambo yaliyopo wala mambo yawezayokuja; hakuna ugonjwa, wala huzuni, wala mauti, wala shida, chochote kiwezacho kututenga sisi na kusudi la Mungu aliye hai.

Kile Mungu alichowaza katika nia Yake, kile Mungu alichokikusudia moyoni mwake ili kitimie, hakuna pepo, hakuna nguvu, hakuna chochote kiwezacho kututenga na mpango huu mkuu wa milele wa Mungu. Itakuwa kama Mungu alivyosema [16]

9

Mungu analokusudi la wewe kuwa hapa. Kama tu unaweza kuwa, ufike pale mahali, utaepusha matatizo mengi kwa Mungu na wewe mwenyewe, pia. [17]

Nukuu za kiingereza:

- (1) “YESU KRISTO yule yule “ (62-0718), Aya 29
- (2) “Matarajio” (53-0507), Aya 23-24
- (3) “Agano lisilo na mashariti” (54-0306), Aya 75 +34
- (4) “kuwa na Imani na Mungu: (54-0900), Aya 8
- (5) “Mungu akikamilisha kanisa lake” (54-1204), Aya 19-20
- (6) “Ugomvi kati ya Mungu na Shetani” (62-0531), Aya 9-10
- (7) “Kristo ni siri” uk 29
- (8) “Uungu wa YESU KRISTO” (49-1225) Aya 80 + 110
- (9) Imani kamilifu (63-0825 E), aya 64-70
- (10) “Muungano usioonekana wa Bibi Arusi” (65-1125), uk 10
- (11) “siku ile pale kalvari” (60-0925), Aya 15/3 – 6
- (12) “Wakati wa kanisa la Smirna” Kitabu cha nyakati 7 sura 4 uk 153
- (13) “Chujio la mtu mwenye busara” (65-0822E), Aya 73

(14) “Maswali na majibu” (64-0830E) Aya, 73

(15) “maji ya kudumu” (61-0723m), Aya 149b – 152

(16) “Ninajua mteteaji wangu anaishi” (58-0406S), Aya 12 -13

(17) “kwa nini unalia Neno” (63-0714M), Aya 43

jiwe la kiroho la kujengea na 164 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306.

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa: Charles E. Y. Kanju,

Box 5138, Tanga

E-mail:

chaelika@hotmail.com

Cell.phone 0784704299